



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



Taarifa namba: 065

09/06/2023

TAARIFA KWA UMMA

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Mji Tunduma chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ayubu Mlimba limefanya maamuzi kwa watumishi waliohusika kwa makosa mbalimbali ya kinidhamu

Mhe. Mlimba amesema baada ya taratibu zote za kinidhamu kufuatwa Baraza la Madiwani ambalo ni Mamlaka ya Nidhamu ya watumishi wa umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma lilijigeuza kuwa kamati ya nidhamu kujadili na kufanya maamudhi kwa watumishi wote ambao walikuwa na tuhuma mbalimbali za makosa ya kinidhamu

Watumishi waliopatikana na hatia ni tisa (09) ambapo Baraza limefanya maamuzi yafuatayo ambayo yamegawanyika katika makundi manne

A. KUKATWA MSHAHARA

- 1) Patricia Mbigili – Mkuu wa Divisheni ya Elimu Sekondari
- 2) Raphael Simkonda – Afisa Mtendaji wa Kata III

Hawa watatumikia adhabu ya kukatwa asilimia kumi na tano (15%) ya mshahara kwa muda wa miaka mitatu (03)

B. KUSHUSHWA CHEO

- 1) Ronald Msangi – Afisa Kilimo I

Huyu atatumikia adhabu ya kushushwa cheo chake

C. KUFUKUZWA KAZI

- 1) Obed Mwakalinga – Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
- 2) Ibrahimu Lulimo – Afisa Manunuzi II
- 3) Ally Farayo – Mahandisi daraja la II
- 4) Dickson Kisenime – Mahandisi daraja la II


Hawa Baraza la Madiwani limeazimia kuwafukuza kazi

D. WATUMISHI WA MKATABA

- 1) Ally Hassan – Msanifu Majengo (Architect)
- 2) Japhet chota – Mkadiriaji Majengo (QS)

Hawa Baraza la Madiwani limeazimia kusitisha mikataba yao na kufukuzwa kazi

Mwisho: Mhe. Mlimba amewaomba watumishi wote kuendelea kuchapa kazi kwa bidii huku wakitanguliza maslahi ya taifa mbele wakifuata Weledi, Maadili na Nidhamu ya kazi. Yeyote atakaye kiuka taratibu za kazi atachukuliwa hatua kali za kinidhamu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma



WILLIAM MAGANGA

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA MJI-TUNDUMA**